•JITAHIDINI KUUTAFUTA USIKU WA LAYLATUL QADRI

•ZAKAATUL FITRI NA HEKIMA YAKE

Mwandishi:

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

Simu: 0715263253

Jitahidini kutafuta Laylatul Qadri (usiku wenye cheo):

Huu ni usiku wenye cheo na daraja kubwa mbele ya Allaah Ta'alaa kwa sababu ni usiku ambao ndani yake imeteremka Qur'an kitabu ambacho ndani yake kuna mwongozo na nuru kwa watu wote, kwa hiyo hii fursa muhimu kwa muislamu kujitahidi kumuomba Mola wake haja zake mbalimbali na kubwa zaidi ni kuomba msamaha wa madhambi yake. Usiku huo unapatikana katika siku kumi mwishoni mwa mwezi wa ramadhani na hiyo ni fadhila ya Allaah kwa umma huu pekee. Hakika ni usiku wenye Baraka nyingi, huteremka ndani yake Malaika akiwemo na Jibril alaihimus salaam na pia ni usiku ambao hupangwa matendo ya waja kwa muda wa mwaka mzima na usiku huo huwa ni salama mpaka asubuhi yake. Mtume swala na salamu zimshukie akijitahidi sana kufanya ibada katika masiku haya kumi na kuwahimiza wakeze na watu wa nyumbani kwake mpaka, akasema hali ya kutuhimiza:

«تَحَرَّوْا لَيْلَةَ القَدْرِ فِي الوِتْرِ، مِنَ العَشْرِ الأَوَاخِرِ مِنْ رَمَضَانَ»

"Itafuteni Laylatul Qadri katika (masiku ya) witri katika siku za mwisho wa ramadhani[1]".

Na wakati alipoulizwa na Aisha Allaah amridhie kuhusu dua ya kusoma endapo ataujua huo usiku wa Laylatul Qadri, akasema:

«قُولِي: اللَّهُمَّ إِنَّكَ عَفُوٌّ تُحِبُّ الْعَفْوَ فَاعْفُ عَنِّي»

"Sema: Ewe Allaah, hakika wewe ni mwingi wa msamaha unapenda kusamehe, basi nisamehe[2]".

[1]- Bukhari (2017) na Muslim (1169).
[2]- Sunan Tirmidh (3513).

Kwa hiyo mtu anatakiwa aisome kwa wingi dua hii katika masiku haya hasa wakati wa usiku lakini haijathibiti ziada ya neno (Karim) kama wanavyo fanya baadhi ya watu, usiseme: اللَّهُمَّ إِنَّكَ عَفُوٌّ كَرِيْمٌ

Pia kuna baadhi ya watu wameifanya dua hii kuwa ni uradi wao wa ramadhani wanaisoma kila baada ya swala ya faradhi kuanzia mwanzo wa ramadhani jambo hili ni bidaa haifai ni sawa mtu atasoma peke yake au kwa sauti ya pamoja.

Ndugu muislamu Allaah Ta'alaa ameuficha kujulikana kwake usiku huo ili watu wajitahidi kufanya ibada kwa ajili ya kuutafuta, kwa kuleta adhkaar, swala na kuomba dua mbalimbali, pia umefichwa usiku huo ili iwe ni mtihani kwao ili ajulikane ni nani miongoni mwao ana pupa zaidi ya kupata rehma za Allaah Subhaanah.

Ndugu muislamu Laylatul Qadri haitokei katika usiku mmoja tu kila mwaka, huenda mwaka huu ikapatikana katika usiku wa tarehe 27 na mwakani ikatokea katika usiku wa 21 n.k, ili watu watoe juhudi katika masiku kumi yote ya mwisho wa ramadhani.

Haikuja Laylatul Qadri ili mtu aombe mambo ya dunia yao kama zile simulizi za zamani za uwongo kwamba Laylatul Qadri ni mwanga mkubwa unaotoka mbinguni na kuenea ardhini mpaka ndani ya majumba na wengine huita Nyota Jaha kwa maana ni nyota yenye utukufu na mtu akipata bahati ya kuiona akaomba atakacho atapata, baadhi yao wakakesha kusubiri Nyota jaha ili waombe magari, nyumba, na mafanikio katika biashara zao n.k! hali ya kuwa Mtume swala na salamu zimshukie amemfunza kipenzi chake Aisha amuombe Allaah msamaha, hii ni ishara kwamba hakuna kitu kikubwa zaidi kusamehewa madhambi.

Zakaatul Fitri (zaka kwa ajili ya kula mchana) na hekima yake:

1. Nini hukumu yake:

Zaka hii ni wajibu kwa kila muislamu, awe mdogo au mkubwa, mwanamme au mwanamke, muungwana au mtumwa, kwa hadithi ya Ibn Umar Allaah amridhie:

«فَرَضَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ زَكَاةَ الفِطْرِ صَاعًا مِنْ تَمْرٍ، أَوْ صَاعًا مِنْ شَعِيرٍ عَلَى العَبْدِ وَالحُرِّ، وَالذَّكَرِ وَالأُنْثَى، وَالصَّغِيرِ وَالكَبِيرِ مِنَ المُسْلِمِينَ»

"Amefaradhisha Mtume swala na salamu zimshukie Zakaatul Fitri pishi ya tende au shairi, juu ya mtumwa na muungwana, mwanamme na mwanamke, mdogo na mkubwa miongoni mwa waislamu[3]".

2. Je ni mwaka gani ilifaradhishwa?

Zakaatul Fitri ilifaradhishwa katika mwezi wa Sha'bani mwaka wa pili wa hijra.

3. Nini hekima yake?

Kutoka kwa Ibn Abbaas Allaah amridhie amesema:

«فَرَضَ رَسُوْلُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ زَكَاةَ الفِطْرِ طُهْرةً لِلصَّائِمِ مِن اللَّغْوِ والرَّفَثِ وَطُعْمَةً لِلْمَسَاكِيْنِ»

"Amefaradhisha Mtume swala na salamu zimshukie Zakaatul Fitri kwa ajili ya kumtwaharisha mfungaji kutokana na maneno machafu na upuuzi na kuwa ni chakula kwa masikini[4]".

[3]- Bukhari (1503), Muslim (984) na wengine.

[4]- Abu Daud (1609), Ibn Maajah (1827) na wengine.

Na pia unatoa kwa ajili ya kushukuru neema ya Allaah juu yako kwa kutekeleza ibada mbalimbali ndani ya mwezi wa ramadhani.

Amesema sheikh Ibn Uthaymiin Allaah amrehemu: **[(mtu anatoa Zakaatul Fitri) kwa ajili ya kudhihirisha shukrani yake kwa Allaah Ta'alaa kwa kula mchana baada ya kukamilisha (funga ya) mwezi wa ramadhani[5]].**

4. Nani inampasa kutoa Zakaatul Fitri?

Masharti ya mtu anaewajibika kutoa Zakaatul Fitri ni mawili:

1) Awe ni muislamu.
2) Awe na chakula cha ziada baada ya chakula cha kumtosheleza yeye na familia yake mchana na usiku wa Idd.

- **Je hutolewa Zakaatul Fitri kwa ajili ya mimba?**

Kundi kubwa la wanachuoni wamesema kwamba haitolewi Zakaatul Fitri kwa ajili ya mimba (mtoto wa matumboni).

- **Je ni sharti mtu awe anamiliki kiwango maalumu?**

Hakuna dalili yenye kufahamisha kwamba mtu anatakiwa kumiliki kiwango maalumu, ndiyo maana maulamaa wanataja sharti la mtu kuwa muislamu na kupata ziada ya chakula chake yeye na familia yake mchana na usiku wake, atatoa kiasi cha kilo 2 na nusu au kilo 3 ya chakula kinacho pendwa zaidi katika mji wake.

Amesema Imam Shaukani Allaah amrehemu: **[Na hii ndio sawa, kwa sababu hadithi zimetaja kwa kuachilia na wala hazijahusisha tajiri au masikini[6]].**

[5]- Al-Fataawa (Jz. 18, Uk. 257).
[6]- Nailul Autwaar (Jz. 4, Uk. 251).

5. Je itafaa kutoa kiasi cha pesa badali ya chakula?

Ama kuhusu kutoa pesa badali ya chakula jambo hili hakuna aliye ruhusu katika maimamu wanne Allaah awarehemu isipokuwa Abu Hanifa pekee.

- Amesema sheikh Ibn Baaz Allaah amrehemu: **[Kauli ya wengi katika maulamaa ni kwamba haifai kutoa kiasi (cha pesa) kwa sababu ni kwenda kinyume na alivyosema Mtume swala na salamu zimshukie na (walivyo fahamu) Maswahaba wake Allaah awaridhie[7]].**
- Amesema sheikh Ibn Uthaymiin Allaah amridhie: **[Haifai kutoa pesa kwa sababu kilicho wajibishwa (kutoa) ni chakula[8]].**

6. Ni wakati gani hutolewa Zakaatul fitri?

Kauli yenye nguvu ni kwamba wakati wa wajibu wa kutoa Zakaatul fitri ni baada ya kuzama jua siku ya mwisho ya ramadhani na wakati bora zaidi ni asubuhi ya siku ya Idd. Kwa hiyo lau kama mtu atasilimu au atazaliwa mtoto kabla ya kuzama jua kwa muda mchache ni wajibu wake kutoa zakaatul fitri, na mwisho wake ni kabla ya kuswaliwa swala ya Iddi.

«فَرَضَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ زَكَاةَ الفِطْرِ... وَأَمَرَ بِهَا أَنْ تُؤَدَّى قَبْلَ خُرُوجِ النَّاسِ إِلَى الصَّلاَةِ»

“Amewajibisha Mtume swala na salamu zimshukie Zakaatul fitri... Na ameamrisha itolewe kabla watu hawajatoka kwenda kuswali”[9].

---

[7]- Al-Fataawa (Jz. 14, Uk. 32).
[8]- Al-Fataawa (Jz. 18, Uk. 265).
[9]- Bukhari (1503) na Muslim (986).

7. Mambo mbalimbali kuhusu Zakaatul Fitri:

1) Hapewi Zakaatul fitri isipokuwa masikini aliye muislamu.
2) Inafaa kumfanya mtu wakala kwa ajili ya kutoa Zakaatul fitri.
3) Inafaa kwa masikini kuwakilishwa katika Zakaatul fitri.
4) Hakuna dua maalumu ya kusoma wakati wa kutoa.
5) Zakaatul fitri hutolewa katika sehemu ambayo itakupata sikukuu ya Iddi hata kama ni mbali na mji wako.
6) Inajuzu kumtolea Zakaatul fitri mtumishi wako wa ndani akiwa ni muislamu na asili ni kuwa atoe yeye mwenyewe.
7) Haifai kumpatia mtumishi wako ila akiwa ni masikini.
8) Inafaa kwa mtu (masikini) aliyepewa Zakaatul fitri kutoa kumpa mtu mwingine ambaye anastahiki na pia inajuzu kwake kuuza kile alichopewa.
9) Akichelewa kutoa Zakaatul fitri kwa udhuru au kwa sababu ya kukosa masikini wa kumpatia hakuna ubaya na atatoa wakati akipata wepesi wa hilo.
10) Itafaa kumpa Zakaatul fitri masikini mmoja hata kama ni chakula cha watu wengi.
11) Mwenye kutoa Zakaatul fitri baada ya swala ya Iddi haitazingatiwa na itakuwa ni sawa na sadaka nyingine.
12) Akichelewa kutoa kwa makusudi atapata dhambi na itamlazimu yeye kulipa.
13) Itafaa kumpa msimamizi wa Zakaatul fitri kwa siku moja au mbili kabla ya kumalizika ramadhani.

Wallaahu a’alam.

Usiku wa 27/ramadhani/14141h – 17/5/2020

Pongwe Tanga.